TANGAZO LA SERIKALI NA. 77 la tarehe 2/2/2024

SHERIA YA USIMAMIZI NA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWENYE GARI MOJA KWA SHIRIKA LA ABBOTT FUND TANZANIA YA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye gari Moja kwa Shirika la Abbott Fund Tanzania ya Mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika tarehe 14 Disemba mwaka 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wote wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa gari moja lililoainishwa kwenye Jedwali linaloingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali kupitia forodha na au kwa niaba ya Shirika la Abbott Fund Tanzania kwaajili ya kutumika katika mradi wa ujenzi wa nyumba za watumishi wa Zahanati ya Bantu, ukarabati na upanuzi wa Shule ya Sekondari ya Mapatano pamoja na utoaji wa huduma za dharula unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha wa ushuru unaotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa, iwapo gari husika litatumika kwa matumizi tofauti au litahamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine asiyestahili kupata manufaa yanayotolewa chini ya Amri hii.

Kuisha kwa muda

4. Amri hii itafikia ukomo tarehe 11 ya mwezi Juni, mwaka 2024.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na | Maelezo | Namba ya Chasesi | Namba ya Injini |
|---|---|---|---|
| 1. | Toyota, Land Cruiser hardtop, Viti Kumi, Milango Mitano | JTEEB71J30-F0248663FJ20-K280519 | IHZ-1040696 |

Dodoma,
23 Januari, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*